

7
MAMBO USIYOYAJUA
KUHUSU DHAMBI
daudi lubeleje

# 7 MAMBO USIYOYAJUA KUHUSU DHAMBI

daudi lubeleje

*I Wathesalonike 4: 2 – 5*

*“2 Kwa kuwa mnajua ni maagizo gani tuliyowapa kwa Bwana Yesu. 3 Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu, mwepukane na uasherati; 4 kila mmoja wenu ajue kuuweza mwili wake katika utakatifu na heshima; 5 si katika hali ya tamaa mbaya, kama Mataifa wasiomjua Mungu.”*

*Kitabu hiki ni kwa mwamini yeyote*

Hakimiliki © Daudi Lubeleje, 2017
Simu: +255 764 771 298, Baruapepe: dlubeleje9@gmail.com

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuhifadhi, kuchapisha kwa njia ya kielektroniki au mekaniki, kutoa vivuli, kurekodi au kubadili sehemu yeyote ya kitabu hiki kwa njia, namna na mfumo wowote bila idhini ya maandishi kutoka kwa mchapishaji.

Sanifu ya kurasa & jalada: DL Bookstore, Arusha Tanzania
Simu: +255787163013, Baruapepe: dlbookstore@zoho.com

ISBN 978 0 7334 2609 4

# YALIYOMO

UTANGULIZI.....................................................................1

JAMBO LA 1: INAOTEA MLANGONI............................................3

JAMBO LA 2: INAKUTAMANI WEWE............................................5

JAMBO LA 3: INAPUNGUZA UTUKUFU WA MUNGU...................9

JAMBO LA 4: IKIKOMAA HUZAA MAUTI.....................................13

JAMBO LA 5: KIZUIZI CHA MEMA...............................................19

JAMBO LA 6: KUONEKANA KITU KICHAFU................................21

JAMBO LA 7: INAFICHA USO WA MUNGU................................25

MAOMBI YA TOBA............................................................................27

KUHUSU MWANDISHI.....................................................................29

VITABU VINGINE...............................................................................31

# UTANGULIZI

Bwana Yesu asifiwe,

Si kwa bahati mbaya kitabu hiki kimekufikia. MAMBO 7 USIYOYAJUA KUHUSU DHAMBI ni kitabu kwa kila mwamini kukisoma. Baada ya kusoma kitabu hiki ni matumaini yangu kupitia mambo haya 7, utapata majibu ya swali hili *“Kwanini yatupasa kutunza utakatifu?”* Hivyo utaongeza bidii yako kumpendeza Mungu katika mwenendo wako wote.

*Kuokoka ni hatua ya kwanza kuliishi kusudi lako. Dhambi ni kikwazo cha kwanza kuharibu kusudi la Mungu katika maisha yako*.

Kitabu hiki kiwe msaada kwako kuongeza chachu ya wewe kutunza kusudi la Mungu kwa kuepuka kuchafuliwa na dhambi, Kumbuka Neno la Mungu lasema *“Msishike, msionje, msiguse” [Wakolosai 2:21]*

**Daudi Lubeleje**

# JAMBO LA 1

*Jambo la kwanza linasema "dhambi inaotea mlangoni". Mwanzo 4:7 ".......Usipotenda vyema dhambi iko, inakuotea mlangoni,..........".*

Mlango ni nafasi ya kuruhusu au kutoruhusu kilicho nje/ndani kuingia/kutoka ndani/nje. Wakati Bwana Yesu anasema *"....nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake,..........." (Ufunuo wa Yohana 3:20),* HALI KADHALIKA, dhambi haiji kupitia dirishani au wapi, bali iko mlangoni na yenyewe ikiotea!.

Kama dhambi inaotea mlangoni, lazima iwe imejificha maana ikija kwa wazi utaiona na huwezi kufungua mlango ikapita. Tofauti na Bwana Yesu hapohapo mlangoni anabisha ili kuingia, haotei kama ilivyo dhambi.

Dhambi inaotea mlangoni kwa sababu hapo ndio sehemu pekee inaweza fanya maigizo kama yenyewe si dhambi vile, bali ni jambo zuri, ni uzima, kwamba ukiruhusu utapata faida na si hasara ila kumbe ni hila za kukuotea!.

Kumbuka *2 Wakorintho 11:14 inasema "........Maana shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru"*. Kujigeuza huku kwa shetani kuwa malaika wa nuru ni kukushawishi ili ufungue mlango, maana dhambi inaotea hapo mlangoni.

Sababu kubwa inayofanya dhambi kuotea mlangoni tunaipata tukisoma *Yohana 10:2 "Aingiaye mlangoni ni mchungaji wa kondoo"* na mchungaji wa kondoo si mwingine ni Yesu Kristo (Yohana 10:11-14). Kama Yesu Kristo huingia mlangoni, na dhambi kwa kuotea hutaka kupitia hapohapo ila ikiisha kujigeuza na kuonekana kama ni jambo la faida.

Kuna baadhi ya mambo katika maisha yetu hususani yale yanayowakumba vijana yanapokuja huonekana ni mema kumbe ni dhambi inaotea mlangoni. Mfano masuala ya mahusiano ni eneo ambalo shetani hufanya mambo yaonekane kama ni ya Mungu kumbe hapana. Mambo kama kufanya tendo la ndoa kabla ya ndoa na wakati si wanandoa ni dhambi, kwa bahati mbaya dhambi huotea hapo, inafanya tendo la ndoa hata kama hamjaingia kwenye ndoa lionekane ni sawa tu.

Tunapaswa kujua si yote yanakuja kwetu ni mema tu! bali mengine ni dhambi inaotea mlangoni. Kwa sababu Yesu Kristo anabisha hapo mlangoni na dhambi inaotea hapo mlangoni ni vema kupima kila jambo kwanza kwa chujio la Neno la Mungu.

# JAMBO LA 2

*Jambo la pili linasema, "Dhambi inakutamani wewe uliyempa Yesu Kristo maisha yako". Tukisoma katika Mwanzo 4:7 "...Usipotenda vyema dhambi iko,..nayo inakutamani wewe...".*

Kutamani kwa lugha rahisi humaanisha *"kutaka sana".* Kila mwamini anapaswa kujua dhambi inamtaka sana na haiwezi kutulia mpaka imempata. Kutamani kwa dhambi huambatana na ushawishi unaoletwa na dhambi yenyewe. Ushawishi huu huficha ubaya wa dhambi. Nitatumia mfano ufuatao kuelezea kutamani kwa dhambi kulivyo;

Tukisoma Mwanzo 3: 1-6, hasa mstari wa 6 inasema *"Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi akatwaa matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala". Angalia! Kwa sababu dhambi iliwatamani Adamu na mkewe, kwa kutumia ushawishi wake, ilifanya mwanamke akaona matunda ya mti waliokatazwa wasile kuwa WAFAA KWA CHAKULA na tena WAPENDEZA MACHO (Mwanzo 2:17).*

Hata leo, kwa yeyote aliyeokoka, dhambi inamtamani, hata kumshawishi kwa kumwonyesha mambo mengi Mungu aliyokataza kuonekana ni mazuri. Vijana wengi leo, kwa kutotambua hilo, wamefanya dhambi na kuanguka huko. Mtume Paulo alisema

*"lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali, inapiga vita na ile sheria ya akili zangu, na kunifanya mateka ya ile sheria ya dhambi iliyo katika viungo vyangu" (Warumi 7:23).*

Kutamani kwa dhambi hufanya hata vita na wewe!, Yale uliyoyaacha baada ya kuokoka, unashangaa dhambi inakutamanisha tena, Sikiliza mtoto wa Mungu!, hiyo ni vita imekuja kwako. Kumbuka hata katika maisha ya kawaida, unapotamani kufanya mambo fulani uliyojiwekea, hutakaa utulie mpaka umefanikiwa. Hata dhambi inatamani, ina kiu ya kumwangusha mtoto wa Mungu, atoke kwenye kusudi la Mungu. *1 Petro 2:11 inasema "...........ziepukeni tamaa za mwili zipiganazo na roho",* Umeona! tamaa za mwili ni matamanio ya dhambi kutimiza lengo lake la kukutamanisha ili umwache Mungu.

Sasa, dhambi inapokutamani, inataka upoteze nafasi yako kwa Mungu uliyopewa. Leo watoto wa Mungu wengi wamepoteza huduma, utakatifu, baraka na mambo mengi lukuki kutoka kwa Mungu, kwa kuifuata dhambi ilipowatamanisha.

Nimalizie kwa kusema hivi, kwa nafasi kubwa dhambi inapomtamani mtoto wa Mungu, hutumia mwili kwake. Tukisoma Warumi 8: 5-11, Wagalatia 5:16-17, 1 Petro 2:11 twapata kujua hili.

Hebu tuamue kujitoa kwa Mungu ki-sawasawa, tunapotembea tujue si yote yanayokuja ni ya Mungu, mengine ni ushawishi wa dhambi hata kama yanapambwa vipi kwa kupendeza. Tafakari mistari ifuatayo na Mungu atusaidie kwa neema yake, kumbuka mimi na wewe ni zaidi ya washindi;

*Warumi 6:13 "Wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi; bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kuwa silaha za haki".*

*Warumi 12:1-2 "...........itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendezam na ukamilifu"*